

- Zungushia utepe wa nailoni wenye upana wa sentimita mbili na nusu kwenye ungio pamoja na kitawi kizima.




#### Utunzaji wa miche

- Mwangilia maji mara baada ya kubebesha na endelea kumwagilia mara moja kwa siku kulingana na hali ya hewa.
- Chunguza dalili za kuchipua vitawi kuanzia wiki ya pili tangu kubebesha
- Ondoa machipukizi yanayoota chini au kwenye ungio.



- Legeza utepe uliozungushwa mara dalili za kitawi kuchipua zinapoonekana ili kuruhusu majani yaote
- Fungua utepe wa ungio mara dalili za utepe kubana sana zinapojitokeza.
- Miche huwa tayari kupandikizwa shambani mara unapokuwa na majani manne au zaidi yaliyokomaa



- Punguza kivuli kwenye kitalu taratibu na hatimaye ondoa kabisa ili kuifanya miche izoee mazingira ya shambani siku tano hadi saba kabla ya kupeleka kupanda shambani.



## UBEBESHAJI WA MICHE YA MIKOROSHO



#### Kimetayarishwa na:

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania  
TARI - Naliendele  
S. L. P. 509,  
MTWARA  
Email : [cdnaliendele@tari.go.tz](mailto:cdnaliendele@tari.go.tz)

## UBEBESHAJI WA MICHE

### Utangulizi

Ubebishaji ni kitendo cha kuunganisha miti miwili ya jamii moja ili iungane na iendelee kukua pamoja kama mti mmoja. Mti unaochangia sehemu ya mizizi huitwa kishina na unaochangia shina huitwa kikonyo au kitawi. Kikonyo kinapatikana kutoka kwenye mti mama wenye sifa nzuri zinazotakiwa.

### Faida za ubebishaji:

- Kupata miche bora yenye kustahimili magojwa, wadudu waharibifu, kuzaa korosho kubwa safi na kutoa mavuno mengi na bora.
- Mikorosho huwahi kutoa maua na kuzaa, katika mwaka wa kwanza tangu kupandwa.
- Mikorosho hairefuki sana hivyo upulizaji wa viuatilifu huwa rahisi.

### Jinsi ya kubebesha

- **Kuandaa vishina**
  - i. Vuna mbegu kutoka kwenye mikorosho yenye sifa za uzaaji mzuri, isiyokuwa na magonjwa ama wadudu waharibifu
  - ii. Panda mbegu kwenye viriba.
  - iii. Vishina huwa tayari kwa kubebesha vinapokuwa na majani matatu au zaidi.

### Kuandaa vitawi (vikonyo)


- Vuna vitawi wakati wa asubuhi .
- Chagua vitawi vyenye rangi ya kikahawia vilivyo komaa na ambavyo havijachipua.
- Hakikisha vitawi na vishina vinakuwa na unene unaolingana.
- Ondoa majani kisha vihifadhi visinyauke kwa kuvifunga kwenye karatasi iliyoloweshwa maji na viweke kwenye mfuko wa plastiki kivulini.

### KUBEBESHA

- Kata kishina juu ya majani mawili kwa kutumia kisu kikali.



- Pasua katikati kiasi cha sentimita mbili na nusu kuelekea chini.



- Pachika kitawi kwenye nafasi ya kishina kilichopasuliwa.
- Oanisha ganda la kitawi na kishina viwe sambamba.



- Chonga pande mbili za kitako cha kitawi kwa mkato wa urefu wa sentimeta mbili na nusu upate umbo la kabari.
- Funga ungio la kishina na kitawi kwa kutumia utepe wa nailoni wenye upana sentimeta moja na nusu au nusu inchi.

